# JUKWAA LA UCHUMI



**HAZARD AMCHANGANYA ZIDANE**

KOCHA wa klabu ya Real Madrid, Zinedine Zidane, amesema...

UK.22

# Ufugaji samaki fursa ya kukuza uchumi wa vijana



CHARLES Makoi akionyesha samakia aliyekaushwa tayari kwa kusafirishwa nje ya nchi.

Na Gift Mongi Moshi

UFUGAJI wa samaki ni njia mojawapo ambayo huinua uchumi wa vijana, kutokanana upatikanaji wa fursa lukuki za ajira ikiwemo kufuga na kuuza.

Ufaguaji wa samaki huwa ni rahisi kufanyika katika eneo lolote, lenye ardhi ya kutosha na upatikanaji wa maji.

Mathalani katika baadhi ya maeneo ya vijijini, wapo vijana waliopata tija kutokana na ufugaji wa samaki.

Goodluck Makoy kijana mfugaji wa samaki aina ya kambale katika Kijiji cha Sambarai, Kata ya Kindi Halmashauri ya Moshi ambapo anasema mradi huo umekuwa na manufaa makubwa kwake na jamii inayomzunguka.

Anasema alianza mradi huo mwaka 2016, amekuwa akiuza samaki na vifaranga anaowatotolesha eneo la mradi.

"Hapa napata faida mara mbili kwa kuuza samaki wenyewe, lakini pia nauza vifaranga kwa ajili ya watu wanaotaka kwenda kufuga,"anasema.

Goodluck anasema hadi sasa wafugaji zaidi ya 400 wamenufaika na mradi huo, kwa kupewa mafunzo ambayo imewawezesha kwenda kuanzisha miradi yao ya ufugaji.

Anasema ufugaji wa kambale ni rahisi na hauna gharama kubwa katika uendeshaji wake na kwamba matokeo yake ni makubwa kutokana na samaki hao kukuwa kwa haraka.

"Hapa tunazalisha vifaranga wengi wasio na idadi hivyo mteja akitaka idadi yoyote ile tunamtayarishia kadri ya uhitaji wake naye akafuge ili ajikwamue kiuchumi, "anasema.

Goodluck anasema katika mradi huo tayari ametoa ajira nne za kudumu na hujitokeza ajira za msimu kipindi cha kuvuna.

**HALI YA SOKO**

Kuhusu hali ya soko mwanzilishi wa mradi huo unaojulikana kama

> **"Hapa napata faida mara mbili kwa kuuza samaki wenyewe, lakini pia nauza vifaranga kwa ajili ya watu wanaotaka kwenda kufuga.**
>
> Goodluck Makoy

Soul Peace Aqua Fish, Charles Makoi anasema hali ya soko la ndani sio nzuri ikilinganishwa na soko la nje.

Anasema ndani ya nchi watu wengi hawapendelei samaki aina ya kambale, wanahitaji zaidi aina nyingine na hivyo kusababisha soko kutokufanya vizuri hapa ndani.

Anasema hivi sasa wanatafuta masoko nje ya nchi yatakayokuwa na uhakika kwa wafugaji wengine ambao bado hawajapata uhakika wa soko.

"Sasa samaki tunao wengi na tumeshawasindika ,tunasubiri vibali ili kusafirisha nje ambapo soko limeonekana ni nzuri zaidi,"anasema.

Anasema waachuzi wamekuwa wakiwalangua wafugaji kwa kutoa pesa zisizoendana na gharama za uzalishaji, jambo ambalo ni linawaumiza wafugaji hao.

"Utaratibu wa kupata vibali umekamilika kwa wafugaji wakianza kuuza samaki hao nje watapata ahueni kwani kutakuwa na uhakika wa soko,"anasema.

Anaiomba serikali kuangalia uwezekano wa uanzishwaji wa kiwanda au cha chakula cha samaki, ili kipatikane kirahisi jambo litakolochochea ufugaji wa samaki kwa wingi.

**FURSA YA UCHUMI**

Rose Mushi mkazi wa Kijiji cha Sambarai, anasema mradi huo wa Soul Peace Aqua Fish umeleta matumaini mapya kwake kutokana kutokana na kumudu kuendesha maisha yake kwa ishara ya kuchuuza samaki.

Anasema msimu wa kuvuna kina mama wengi hupata ajira za muda kwa kujishughulisha katika uchuuzi na kuwauzia wageni wanaotoka mijini.

"Hapa nanunua kwa bei ndogo wakija wa mjini, nawauzia kwa bei kubwa,hii huniwezesha kutengeneza kipato changu cha kujikimu "anasema.

Alex Kimath dereva wa pikipiki kijijini hapo, anasema msimu wa mavuno kunakuwepo ongezeko la abiria jambo linalompa matumaini ya kuongeza kipato.

"Wakati wa mavuno huwa ninakuwa na vifungashio nawauzia wageni wanaokuja kuchukua kitoweo, kama ilivyo fursa ni pamoja na kujiongeza katika kufikiri,"anasema.

Ofisa uvuvi wa Kanda ya Kaskazini chini ya Wizara ya Mifugo na Uvuvi Rafael Mahinya anasema ufugaji wa samaki ni fursa mpya ya kukuza uchumi, ambayo vijana wengi wanapaswa kukimbilia.

Anasema katika Mkoa wa Kilimanjaro wamekuwa wakiwatembelea wafugaji hao na kuwapa elimu, ili wafuge kwa tija kwa ajili ya soko la uhakika.

"Wafugaji wapo na tunatambua mchango wao kwa kweli na huu ufugaji haupotezi muda kama aina nyingine ya kufuga, "anasema.

Anasema katika kuendeleza kukuza uchumi zaidi, ni wajibu wa vijana kuangalia fursa zinazojitokeza kama ilivyo kwa ufugaji wa samaki, ambapo mtaji wake ni kidogo na matokeo ni makubwa ili kushiriki katika kujenga nchi.



SAMAKI waliokaushwa.

Scanned with CamScanner

UHURU UK 16.

**Lengo>>** Kuhakikisha mifugo inakuwa salama dhidi ya magonjwa

# Serikali yatangaza bei elekezi chanjo za mifugo

**Na JUMBE ISMAILLY,** *Mkalama*

WIZARA ya Mifugo na Uvuvi imetangaza bei elekezi za gharama za chanjo mbalimbali za mifugo na kusema ni wajibu wa kila mdau wa mifugo kuzizingatia.

Akitangaza bei hizo juzi kwenye uzinduzi wa kampeni ya kitaifa ya chanjo ya ugonjwa wa homa ya mapafu, Mkurugenzi wa Huduma za Mifugo, Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Hezron Nonga, alisema bei hizo elekezi za chanjo zilishatangazwa tangu Mei 13, mwaka huu, hivyo ni jukumu la kila mdau wa mifugo kuzizingatia.

Kwa mujibu wa Nonga, bei ya chanjo ya ugonjwa wa homa ya mapafu ya ng'ombe ni sh. 550, chambavu sh. 800, kimeta sh. 500, kutupa mimba sh. 1,500, mdondo sh. 50, mapele ya ngozi, sh. 600 na homa ya bonde la ufa sh. 700.

Chanjo zingine ni ndigana kali sh.17,000, kichaa cha mbwa sh. 1,500, ugonjwa wa miguu na midomo sh. 3,000, sotoka kwa mbuzi na kondoo sh. 3,500, mchanganyiko wa chambavu na kimeta (Tecoblax) kwa mbuzi na kondoo sh. 500 na homa ya mapafu ya mbuzi sh. 3,50.

Mkurugenzi huyo alisisitiza kuwa magonjwa mengi ya mifugo ni yale yanayoambukiza na iwapo hakuna kinga madhubuti ambayo yanaweza kuenea kwa haraka na kusababisha hasara kubwa kwa mfugaji.

Nonga alitaja kinga nyingine madhubuti dhidi ya magonjwa 13 ya kipaumbele ikiwemo CBPPP,CCPP,FMD,LSD, brucellosisi, kimeta, sotoka ya mbuzi na kondoo (PPR), ndigana kali, mdondo, kichaa cha mbwa, homa ya bonde la ufa, homa kali ya nguruwe na chambavu ni chanjo.

"Kuchanja ni njia ya uhakika ya kulinda afya ya mifugo, chanjo hudhibiti magonjwa yasiyoweza kutibika hususan yanayotolewa kwa njia ya mlipuko na kuongeza kuzaliana kwa mifugo na kukua haraka," alisisitiza.

Naye Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Luhaga Mpina aliiagiza Bodi ya Nyama Tanzania na kamati za dawati la sekta binafsi kwamba ifikapo Desemba,mwaka huu kiwanda cha kuchakata nyama ya kuku kiwe kimejengwa mkoani Singida na wananchi wapate huduma hiyo.

Alisisitiza serikali ya awamu ya tano imejenga viwanda vikubwa kuliko hicho kitakachojengwa mkoani Singida, hivyo ni imani yake kwamba ujenzi wa kiwanda hicho hautashindikana kwa muda alioutoa.

"Tumeona hapa uzalishaji mkubwa sana wa kuku katika Mkoa wa Singida ambao umefikia kuku milioni 2.6 ni uzalishaji mkubwa sana wa kuku. Naagiza mambo mawili Bodi ya nyama na kamati za dawati la sekta binafsi kuwezesha kujengwa kiwanda cha kuchakata nyama ya kuku katika mkoani hapa," alisisitiza Waziri Mpina.

Ofisa Maendeleo ya Mifugo wa Halmashauri ya Wilaya ya Mkalama, Elias Mbwambo, alisema licha ya kuwa na upungufu wa watumishi lakini wilaya hiyo ina ng'ombe 130,239, mbuzi 87,986, kondoo 44,673, nguruwe 3,606, punda 10,529, mbwa 10,028 na kuku 308,188.

Msajili wa Bodi ya Nyama Tanzania, Imani Sichwalwe, alibainisha kuwa uwepo wa idadi kubwa ya mifugo hauwezi kusaidia, badala yake kinachotakiwa ni kuiboresha na kuitafutia masoko kwenda nje ya nchi.

## MSAADA

Scanned with CamScanner